

Ndugu Marafiki,

Tumepokea baadhi ya habari zenye kusikitisha leo kuhusu amri ya utendaji ya Raisi Trump inayohusu masuala ya Wakimbizi. Kama ulikuja Marekani ukiwa mkimbizi, maagizo yake mapya wala hayata kuathiri wewe moja kwa moja isipokuwa ikiwa kama una familia au marafiki ambao wamekubaliwa kama wakimbizi na wanatarajia kusafiri kuja Marekani hao ndio watakao athirika.

Kwa sababu kuna ripoti nyingi tofauti na fununu mbalimbali katika jamii, kwa hiyo tunapendelea kutoa baadhi ya miongozo iliyo wazi kwa ajili ya wewe kama unaitaji kuelewa nini maana ya amri hii kwako na familia yako.

### **Amri ya Utendaji ya Raisi Trump Kuhusu Wakimbizi Inasema Nini:**

- Hakuna wakimbizi wapya watakao ruhuswa kuingia nchini Marekani ndani ya siku 120, wakati huku serikali ya Marekani ikiwa na tathmini taratibu zake za kiusalama katika nchi za nje.
- Jumla ya idadi ya wakimbizi watakaopewa hifadhi mwaka huu nchini Marekani itakuwa 50,000 badala ya 110,000
- Raisi Trump amesimamisha kikamilifu mpango wa kuwapa makazi wakimbizi wa Siria angalau kwa wakati huu; hatujuwi kama au wakati gani yeye (au Raisi atakaye kuja baadae) ataanzisha mpango wa makazi mapya kwa watu hawa.
- Amri hii pia inapiga marufuku kwa watu binafsi kutoka katika nchi zifatazo kuingia nchini ndani ya siku 90. Nchi hizo ni pamoja na Siria, Libia, Somalia, na Yemen. Na baada ya siku 90, amri hii ya marufuku yaweza kuelekezwa kwa baadhi ya watu.
- Wakati mwingine baada ya siku 120, serikali ya Marekani itaamua kuacha kutoa hifadhi ya makazi mapya kwa wakimbizi watakaoingia nchini wakitokea kwenye orodha ya nchi mpya zitakazo tangazwa hapo badae. Hatutaweza kujua ni nchi gani hadi pale serikali yenyewe itakapotoa tangazo.

### **Hili Lina Maanisha Nini kwa Wakimbizi Waliopo Ndani Nchini Marekani :**

- Wakimbizi waliopo hapa nchini Marekani wako salama na wanalindwa na sheria ya Marekani na wana haki sawa na wajibu kama raia wa Marekani.
- Hadhi ya ukimbizi haina mwisho, lakini tunawatia moyo wakimbizi wote watume maombi kwa ajili ya kupata kadi ya kijani au kadi ya makazi ya kudumu (Green Card) baada ya mwaka 1 na mwishowe kuomba kuwa raia (baada ya miaka 5).
- Raia wote wa Iraq, Libia, Somalia, Sudan, Siria, na Yemen wanaoishi hapa nchini hawapaswi kusafiri nje ya nchi kwa wakati huu ikiwa hawana uraia wa Marekani. Ushauri huu ni pamoja na wale ambao wanamiliki kadi ya kijani yaani Green Card (kisheria wakazi wa kudumu). Kwa raia wasio raia wa nchi husika, kuweni waangalifu kabla ya kuamua kwenda nchini humo. Ni vyema kuweza kuzungumza na mwakilishi wa idara ya haki au mwanasheria wa uhamiaji kuhusu hali yako.
- Kama una familia au marafiki ambao ni wakimbizi na wanajaribu kuja Marekani, wala usikate tamaa badala yake kuwa na matumaini kwamba watakuja. Lakini unapaswa kujiandaa mwenyewe kwa ajili ya habari gumu au kwa kuchelewa kwa muda mrefu.

Shirika la World Relief litaendelea kuangalia kwa makini mabadiliko yoyote mapya ya serikali yanayoathiri mpango wa makazi mapya ya wakimbizi. Mwezi Mei, tutashiriki habari yoyote inayohusu kufunguliwa upya mpango wa wakimbizi na pia mabadiliko yoyote ya orodha ya nchi zitakazo ruhuswa kupewa makazi mapya.

Bila kujali nini kitatokea katika siku zijazo, tunaendelea kusimama imara na wakimbizi pamoja na wahamiaji. Sisi tuna kupenda, tunaamini katika wewe, na tutakusaidia na kukulinda katika kila njia tuwezayo.